

MWAKA 2021 UWE NI MWAKA WA WATEULE

KUEPUKA KABISA LAANA YA TORATI

Maandiko: Kutoka 16: 1 – 33 na Gal. 3: 13 – 14

1. UTANGULIZI

Kabla ya torati (zile amri kuwekwa wakati wa safari ya wana wa Israeli jangwani) huko nyuma tangu Ibrahimu hadi Yusufu watu (watoto) walikuwa wanagombania matamko ya baraka (maneno) yanayotamkwa juu yao na wazazi wao, wakiamini kabisa kwamba matamko hayo yaliyotamkwa juu yao ni Mungu Baba wa Mbinguni tayari amewabariki. Mtoto alipotamkiwa Baraka na mzazi wake, au Mungu alipotamka Baraka juu ya mtu, mtu huyo tangu siku hiyo alijihesabu kuwa ni mbarikiwa na alianza kutembea kama mtu aliyebarikiwa na Mungu. ***Mwanzo 27: 30 – 40; Mwanzo 32: 24 – 30, 48: 8 – 20 (49: 1 – 28) hata Mwaz 9: 17 – 29.***

- Kamwe hutaona kabisa wakigombania urithi wa nyumba au mashamba ya Baba zao au magari, au ng'ombe au kondoo au fedha au dhahabu!! Waligombania matamko ya wazazi wao, waliyathamini sana matamko ya baraka yaliyotamkwa juu yao na Mungu.

2. Torati ya Musa yenyewe ikaja na urithi wa **vitu** au **mali** zinazoonekana kabisa kwa macho haya ya mwili. **Hali hii ya urithi wa vitu au mali ikawafanya watu wazima waanze kuishi kama fisi wanaongojea daima mzoga unaosazwa na simba badala ya wao kuwinda mnyama wao wenyewe. Torati ikawajenga watu kusubiri vitu vya Bure, mana ya Bure, Kware wa Bure, maji ya Bure, na hata walipoingia nchi ya ahadi, mashamba ya Bure. Hali hii ya kuongojea vitu vya bure ikaathiri ufahamu wao na kupelekea watu kuwa wavivu na wanung'unikaji (walalamikaji) pindi vitu vya bure**

vinapokosekana. Luka 15: 11 - 12 (Hesab 27: 8 - 11) Hes 36: 9 na kwa kizazi cha Torati matamko ya Baraka ya kutamkiwa na Mungu au Baba zao ukabaki kama wimbo tu mzuri uliozoeleka na muda wote wakataka wazazi wao wawape urithi unaowaangukia.

- Nataka kusema kweli leo; maisha haya ya miaka **40** ya wana wa Israeli ya kungojea mana ya bure, Kware (nyama za bure) maji ya bure viliwafanya wana wa Israeli akili zao kupumbaa na kuwafanya waishi maisha tegemezi kwa Musa na YOSHUA hadi walipofunguliwa ufahamu wao baadae. **Yosh 5: 1 - 15 *12 - 15**
- YOSHUA akaanza kuwaelekeza wana wa Israeli jinsi ya kumtegemea Mungu kwa asilimia mia moja na kuwaambia dhahiri kwamba **baraka** zao na **ushindi** wao na **mafanikio** yao zitatoka kwa Mungu mwenyewe endapo watamwamini na kumtazama yeye badala ya kuwatazama wanadamu. **Yer 17: 5 - 8. Jambo hili ndilo lilikuwa chanzo cha kuwafanya wana wa Israel waanze kujibidisha sana katika kumtafuta Mungu na kufanya kazi za mikono kwa bidii na tangia wakati huo Taifa la Israeli likabadilika na kuwa tishio kwa mataifa mengine.**

3. Mwaka 2021 ni mwaka wa kukataa laana ya Torati; ni mwaka wa kila mteule **kujibidisha** sana kumtafuta Mungu kibinafsi na kufanya kazi kwa bidii maadamu Baraka zetu zote zimejumuishwa ndani ya wokovu tulioupata kwa gharama kubwa aliyoilipa Yesu Kristo pale msalabani; ikiwa ni **utajiri - 2Kor 8: 9, ikiwa ni uponyaji 1Petro 2: 24, ikiwa ni mamlaka. Luka 17: 19, Mark 16: 18 n.k**

- Pasipo kutambua kwamba **msalaba** ndiyo asili ya baraka zangu zote na mema mengine ikiwa ni pamoja na marupurupu yatupasayo watakatifu baada ya kuokoka; tutabakia kuwa

wateule wa **kukodoakodoa macho** kwa baraka za watu wengine ili waturithishe wangali hai au baada ya kufa.

- **Nasema leo dhahiri kwamba baraka za kila mmoja wetu na urithi wa kila mmoja wetu tayari Yesu alishatutumkia; kazi yetu ni kung'angana na matamko aliyotutumkia Yesu na kuyaamini na hizi ndizo baraka ambazo hazina majuto wala kugombana na ndugu. Sikia Mungu alivyomwambia Yoshua baada ya ya Musa kufa. *Yosh 1: 1 – 9 *8 – 9*. Yoshua akaishi kwa imani na kuwafundisha watu wale wale kujibidisha na kumtafuta Mungu na kufanya kazi kwa bidii. **Safari nzima wakati wa Yoshua hutasikia wana wa Israeli wakidai mana, au nyama, au maji, wao wanadai wajibu tu basi!!** *Yosh 1: 12 – 18***

4. **Mwisho:** Ndugu zangu tuliookoka, kuendelea hata sasa kufikiria/ kujitegemea urithi wa nyumba za wazazi wetu au mashamba yao au magari yao au fedha zao au dhahabu zao au mifugo yao ni kuendelea **kuathirika kiroho na kiufahamu** na tutaendelea kuishi maisha kama ya fisi ya omba omba kwa watu wengine, lakini zaidi sana hatutakaa **tutambue** kabisa sisi wenyewe faida ya Yesu Kristo kufa pale msalabani na mwisho tutaenda kuishi maisha ya **utoto** wakati tumejazwa Roho Mtakatifu. **Mana ilishakoma tufanye kazi kwa bidii – 2Thes 3: 6 – 12. Bure alikwisha kufa na akazikwa miaka mingi. 2021 TUKATAE KABISA JINA LA CHAKUPEWA, TUWE AKINA CHA KUTOA. TUZIKE FIKRA HIZI POTOFU ZA KUNGOJEA KURITHI VITU VYA MAREHEMU.**

5. Mwaka **2021** uwe ni mwaka wa kung'ngana na matamko yanayotamkwa juu yetu na wazazi wetu wa kiroho na kuyaishi/ kuyatenda kama tunataka kuona mambo ya kutushangaza katika safari hii. Amina.

Na

Askofu Dr. L. M. Mwizarubi

03/01/2021